

# جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

## مشروع تعلم الإسلام - أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 5

الدرس الخامس

### MAANA YA KALIMAT TAUHEED "LAAILAAHA ILLALLAH"

Kalimat "LAAILAAHA ILLALLAH" ndio msingi wa dini, neno hili lina nafasi kubwa sana katika dini ya kiislamu, kwani ndio nguzo ya kwanza katika nguzo za uislamu, pia ni sehemu katika sehemu za Imani, na kukubalika kwa matendo mema kwa kutamkwa Laailaha Illallah, kujua maana yake na kufanya kazi muktadha wake. Ama maana ya haki ambayo haifaifahi kupindisha ni HAPANA MWENYE KUABUDIWA KWA HAKI ILA ALLAH, nayo ni kumpwekesha Allah peke yake katika Ibada, na kuacha Ibada isiyokuwa ya Allah (sw). Mionganoni mwa makosa ya kauli ni kwamba maana ya LAAILAAHA ILLALLAH, hapana muumba isipokuwa ni ALLAH, au hapana muweza au hapana alieanzisha isipokuwa ni Allah, au hakuna yeote mwenye kupatikana isipokuwa ni Allah.

### NGUZO ZA KALIMAT LAAILAAHA ILLALLAH.

Neno hili lina nguzo mbili ;

1. Nguzo ya kwanza ni kukataa.
2. Nguzo ya pili ni kukubali (Kuthibitisha).

Nguzo ya kwanza kukataa, ni kauli ya kusema "LAAILAAHA" nako ni kukataa uungu wa kila kitu hapa duniani.

Pili kukubali (kuthibitisha) ya kuwa hakuna mola isipokuwa ni Allah peke yake asiyeokuwa na mshirika.

Hakuna mola anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Allah (sw), na wala haifai kufanya chochote katika aina za Ibada kwa asiyeokuwa Allah (sw), kwani mwenye kulisema neno hili la LAAILAAHA ILLALLAH akalijua maana yake, akaujua muktadhma wake ya kuwa ni kujiepusha na shirki na kuthibitisha upweke wake Allah (sw) pamoja na kuitakidi kisawasawa ndani ya moyo wake, na kulifanya kazi kwa mwenye kusema hayo, basi huyo atakuwa ni muislamu wa kweli.

Lakini mwenye kulifanya kazi neno hili bila ya kuitakidi kwenye moyo wake, basi huyo atakuwa mnafiki, na mwenye kufanya kinyume ya hayo atakuwa mshirikina kafiri hata kama atalisema hili neno kwenye ulimi wake.

### UBORA WA KALIMAT TAUHEED "LAAILAAHA ILLALLAH"

Neno hili "LAAILAAHA ILLALLAH" lina fadhila kubwa na faida nyingi, mionganoni mwa fadhila zake ;

1. Neno hili ni sababu ya kumzuia mtu asikae milele motoni, kwa yule anaestahiki kuingia motoni mionganoni mwa watu wa tauheed.

فِي الْحَدِيثِ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ - ﷺ - قَالَ: «يَخْرُجُ مِنَ النَّارِ مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَفِي قَلْبِهِ وَزْنٌ شَعِيرَةٌ مِّنْ خَيْرٍ ، وَيَخْرُجُ مِنَ النَّارِ مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، وَفِي قَلْبِهِ وَزْنٌ بُرَّةٌ مِّنْ خَيْرٍ ، وَيَخْرُجُ مِنَ النَّارِ مَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، وَفِي قَلْبِهِ وَزْنٌ ذَرَّةٌ مِّنْ خَيْرٍ» [سنن عبادة: ٤٤ - ١٩٣].

Katika Hadithi ya bwana Mtume (saw) anasema : ("Atatoka motoni yule mwenye kuitamka kalima ya LAAILAAHA ILLALLAH, na kwenye moyo wake ana uzito wa chembe ndogo ya kheri, atatoka motoni mwenye kusema LAAILAAHA ILLALLAH na kwenye moyo wake kuna punje ndogo ya kheri") ( Ameipokea Bukhar na Muslim).

2. Kwa ajili ya neno hili la tauheed, Allah (sw) amewaumba majini na wanadamu, Allah anasema :

قال الله تعالى: (وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّاً وَالْإِنْسَانَ إِلَّا لِيَعْبُدُونَ) [الذاريات: ٥٦]

( " Sikuwaumba majini na wanadamu isipokuwa kwa lengo la kuniabudu" ) (al-Dhariyat:56). (yaani kunipwekesha)

3. Kwa neno hili Allah (sw) aliwatuma mitume wake na akateremsha vitabu kwa mitume.

قال تعالى: (وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونَ) [الأنبياء: ٢٥]

Allah (sw) anasema : (" Hatukutuma mtume yoyote kabla yako, isipokuwa tulimfunulia kwa kumpatia kitabu ya kwamba hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa mimi, basi niabuduni") (Al-Anbiyah:25).

4. Neno hili ndio ilikuwa ufunguo wa mitume kwenye Da'awa yao, ndilo neno la kwanza katika kulingania mitume, kila mtume alisema kuwaambia watu.

... يَا قَوْمَ اَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ﴿٥٩﴾ [الأعراف: 59]

(" Enyi watu muabuduni Allah, hamna nyinyi mungu mwengine Zaidi yake yeye") (Al-A'raf:59).